



TAARIFA KWA UMMA

SIKU YA KIMATAIFA YA WANAWAKE– 2019

Siku ya Kimataifa ya Wanawake (International Women’s Day) huadhimishwa Machi 8 ya kila mwaka. Siku hii ambayo imekuwa ikiadhimishwa na nchi za Urusi kuanzia mwaka 1917 ilitangazwa na Umoja wa Mataifa kuwa SIKU YA KIMATAIFA YA WANAWAKE kuanzia mwaka 1975.

Siku hii inalenga kutambua mafanikio ya mwanamke bila kuangalia rangi yake, dini, kabila au siasa ikiwa ni pamoja na kutafakari maendeleo ya mwanamke na namna ya kuendelea kujikwamua katika matatizo na changamoto zinazokuwa vikwazo vya yeye kujitegemea kifikra, kiuchumi, n.k.

Kwa kutambua umuhimu wa siku hii pamoja na umuhimu wa mchango wa mwanamke katika mapambano dhidi ya rushwa, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) inachukua fursa hii kutamka kuwa inaunga mkono juhudi zinazoendelea duniani kote za kuhakikisha wanawake wanalindwa na inapinga unyanyasaji na udhalilishaji wa aina yoyote ile unaofanywa dhidi ya wanawake ikiwemo kulazimishwa kutoa RUSHWA YA NGONO. Hii ni hatua muhimu kwa TAKUKURU na JAMII katika harakati za KUIMARISHA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA.

Katika siku za hivi karibuni, zimeibuliwa tuhuma nyingi katika jamii zinazohusu RUSHWA YA NGONO zilizoambatana na matukio ya TAKUKURU kuwakamata waliodaiwa kuomba RUSHWA YA NGONO. Kwa kipindi cha 2015/2018 tumepokea na kufanya chunguzi dhidi ya malalamiko **09** yanayohusu RUSHWA YA NGONO ambapo kati ya hizo kesi **5** zilishafikishwa mahakamani na kutolewa hukumu.

Kufuatia matukio haya na kwa kutambua mchango wa wanawake katika kuliletea Taifa letu maendeleo na kupambana na rushwa, kuanzia sasa TAKUKURU itakuwa na Dawati Maalum litakaloshughukia RUSHWA YA NGONO katika ofisi zake zote. Kupitia Dawati hili tutaelimisha na kuhamasisha zaidi umma kuwa na ujasiri wa kutoa taarifa na kupinga vitendo vya RUSHWA YA NGONO na hivyo kupunguza au kuondoa kabisa kero hii ambayo kwa kiwango kikubwa inawaathiri wananchi wa jinsia ya kike.

Tumepanua wigo wa mawasiliano yetu na wananchi ambapo sasa TAKUKURU imefungua kurasa za Tweeter: **TAKUKURU.TZ**; Instagram: **takukuru.tz** na Facebook: **Takukuru Tz**.

Nawasahi wananchi kutumia fursa hizi kuwafichua wadhalimu wanaodai RUSHWA YA NGONO na rushwa nyingine ili kwa ushirikiano huo tukomeshe vitendo hivyo.

RUSHWA YA NGONO ni kitendo cha mtu kutumia madaraka au dhamana aliyopewa kuomba au kulazimisha tendo au upendeleo wa kingono kutoka kwa mtu anayetaka kumhudumia kikazi. Sheria ya Kuzuia na Kupambana namba 11 ya mwaka 2007 imetamka kosa hili chini ya kifungu cha 25 ambapo kwa tafsiri isiyo rasmi kifungu hiki kinasema: *“Mtu yeyote ambaye kwa kutumia nafasi yake au mamlaka yake katika kutekeleza majukumu yake anadai au analazimisha upendeleo wa kingono au upendeleo mwingine wowote kama kigezo cha kutoa ajira, kupandisha cheo, kutoa haki au upendeleo wowote unaotambulika kisheria atakuwa ametenda kosa.”*

Kwa maelezo hayo na kwa kuadhimisha SIKU YA KIMATAIFA YA WANAWAKE kwa mwaka 2019, yenye Kauli Mbiu isemayo ‘BADILI FIKRA KUFIKIA USAWA WA KIJINSIA KWA MAENDELEO ENDELEVU’. Mkurugenzi Mkuu na watumishi wote wa TAKUKURU tunasema **‘BADILI FIKRA, RUSHWA YA NGONO HAIKUBALIKI - TUWAUMBUE’**.

Haya shime kila mmoja wetu popote alipo aunge mkono jitihada za Serikali za kuzuia na kupambana na rushwa ikiwemo RUSHWA YA NGONO kwa kutoa taarifa sahihi za wale wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa ili kwa pamoja tuidhibiti kero hii pamoja na kero nyingine zinazodidimiza maendeleo ya Taifa letu.

Imetolewa na
CP. DIWANI ATHUMANI
MKURUGENZI MKUU - MACHI 7, 2019